TEKINOLOJIA ILIYOBORESHWA YA KUTUMIA MIFUKO ISIYORUHUSU HEWA KUHIFADHI MAZAO

Utangulizi

Uhifadhi bora wa mazao bado ni changamoto kwa wakulima wadogo nchini Tanzania. Kwa kila Kilo 100 za mavuno ya mkulima yaliyohifadhiwa, Kilo 15-25 hupotea.

MIFUKO ILIYOBORESHWA KUHIFADHI MAZAO

- Mifuko iliyoboreshwa kuhifadhi mazao ni aina ya vifungashio visivyo ruhusu hewa.
- Mazao yakijazwa kwenye mfuko na kufungwa vizuri, hewa hupungua na hivyo kusababisha wadudu kuangamia.
- Kuna aina tofauti za mifuko hii ambayo kawaida ina mfuko mmoja au miwili laini kwa ndani.



Aina tofauti za mifuko iliyoboresha ya kuhifadhi mazao

JINSI YA KUTUMIA

- Nunua mifuko iliyoboreshwa kutoka kwa wauzaji waliopendekezwa.
- Kausha mazao kama inavyostahili, kwa mfano; kiwango cha unyevu kisizidi asilimia 13.5 kwa mahindi, 12 kwa mtama, 14 kwa maharage, 13 kwa kunde na mbaazi, na 5 kwa karanga.
- Pepeta kwenye chekeche ili kuondoa uchafu, mchanga na kadhalika.
- Jaribu mfuko kabla ya kujaza nafaka ili kuhakikisha ya kwamba haupitishi hewa. Njia rahisi ni kwa kujaza hewa na kubana mfuko kwa mikano. Usitumie iwapo utapitisha hewa.
- Jaza nafaka kwenye mfuko:
  1. Mimina kiasi kidogo cha nafaka kwenye mfuko wa ndani.
  2. Ingiza mfuko wenye kiasi kidogo cha nafaka kwenye mfuko wa pili au mfuko wa nje.
  3. Ongeza kipimo cha nafaka kufikia ujazo ulioshauriwa.
  4. Funga kwa makini mfuko wa ndani wenye nafaka kwa kutumia kamba.
  5. Funga kwa makini kwa pamoja mifuko yote mmoja baada ya mwingine pia kwa kutumia Kamba.

Na.1
Mimina kiasi kidogo cha nafaka kwenye mfuko wa ndani.

Na.2
Ingiza mfuko wenye kiasi kidogo cha nafaka kwenye mfuko wa pili au mfuko wa nje

Na.3
Ongeza kipimo cha nafaka kufikia ujazo ulioshauriwa

Na.4
Funga kwa makini mfuko wa ndani wenye nafaka kwa kutumia kamba

5. Funga kwa makini kwa pamoja mifuko yote mmoja baada ya mwingine pia kwa kutumia Kamba.

ANGALIZO: Hakikisha unahifadhi mfuko huu juu ya mbao kuzuia unyevu.

Mfano wa mkulima anyetumia mifuko iliyoboreshwa

FAIDA ZA KUTUMIA MIFUKO ILIYO BORESHWA KUHIFADHI NAFAKA

- Hupunguza upotevu wa mazao kwenye hifadhi kwa zaidi ya asilimia 95; hivyo basi uhakika wa chakuka kingi zaidi kwa familia au biashara kwa bei nzuri.
- Hutumika miaka 3 hadi 4 kutegemeana na utunzaji wake.
- Huokoa gharama za uhifadhi.
- Haitumii kemikali yeyote.
- Hupunguza sumu kuvu wakati wa kuhifadhi.
- Walaji kufaidika kwa kupata chakula bora na salama.

MLINGANISHO WA GHARAMA NA FAIDA KWA MFUMO WA KUHIFADHI NAFAKA KWA KUTUMIA VIUATILIFU

MWAKA	Gharama	Mfuko ya kawaida na viuatilifu	Mifuko iliyoboreshwa
1	Mfuko	TSh700	TSh5,000
	Kamba ya kufungia (mara 1)	TSh200	TSh200
	Viuatilifu (mara ya 1)	TSh1,000	TSh0
	Nguvu kazi (mara ya 1)	TSh1,000	TSh1,000
	Viuatilifu (mara ya 2)	TSh1,000	TSh0
	Nguvu kazi (mara ya 2)	TSh1,000	TSh0
	Kamba ya kufungia (mara 2)	TSh200	
2	Mfuko	TSh700	TSh0
	Kamba ya kufungia	TSh200	TSh200
	Viuatilifu (mara ya 1)	TSh1,000	TSh0
	Nguvu kazi (mara ya 1)	TSh1,000	TSh1,000
	Viuatilifu (mara ya 2)	TSh1,000	TSh0
	Nguvu kazi (mara ya 2)	TSh1,000	TSh0
	Kamba ya kufungia (mara 2)	TSh200	
3	Mfuko	TSh700	TSh0
	Kamba ya kufungia	TSh200	TSh200
	Viuatilifu (mara ya 1)	TSh1,000	TSh0
	Nguvu kazi (mara ya 1)	TSh1,000	TSh1,000
	Viuatilifu (mara ya 2)	TSh1,000	TSh0
	Nguvu kazi (mara ya 2)	TSh1,000	TSh0
	Kamba ya kufungia (mara 2)	TSh200	
	Jumla (Gunia 1)	TSh15,300	TSh8,600
	Jumla (Magunia 5)	TSh76,500	TSh43,000

Mfano wa mavuno ya mahindi kwa mkulima anayehifadhi magunia 5 ya kilo 100 kila moja

TAHADHARI

1. Hakikisha mazao yako yamekauka vizuri.
2. Zuia panya kwa kutumia mtego wa panya au paka.
3. Hakikisha sehemu ya ghala la kuhifadhi nafaka ni safi na salama. Tumia kinga za kuzuia wadudu waharibifu ghalani kama vile mitego ya kunasa panya.



Aina za mitego ya panya ambayo hupatikana kwa urahisi

Washirika

Kuhusu Africa RISING

Mpango wa kilimo endelevu Afrika kwa kifupi 'Africa RISING' unajumuisha tafiti tatu za miradi ya maendeleo ambayo inafadhiliwa na shirika la Marekani la Maendeleo ya kimataifa (USAID) kama sehemu ya mpango wa serikali ya Marekani wa kuboresha usalama wa chakula "Feed the Future".

Kupitia utafiti wa vitendo na ushirika wa maendeleo unaofanywa na Afrika RISING, umepelekea kujenga fursa kwa wakulima wa kaya maskini kuondokana na umaskini, kupitia mfumo wa kilimo endelevu. Mfumo huo unaboresha chakula, lishe na usalama wa mapato, haswa kwa wanawake na watoto; na kuhifadhi au kuongeza msingi wa rasilimali asilia.

Miradi mitatu inaongozwa na Taasisi ya Kimataifa ya kilimo kwenye ukanda wa Tropiki (Magharibi, Mashariki na Kusini Afrika) na Taasisi ya utafiti wa mifugo ya Kimataifa (katika nyanda za juu za Ethiopia). Taasisi ya kimataifa ya Sera ya chakula inahusika sambamba kuongoza mradi katika kufuatilia na kutathimini maendeleo ya mradi na athari zake.